

HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

Simu: 028-2220226, 028-22202231

Fax : 028-2220226

Barua pepe: md@bukobamc.go.tz

Tovuti: www.bukobamc.go.tz



S.L.P 284,
BUKOKA,
TANZANIA.

Kumb.Na. BMC/E.50/11/VOL.VIII/11

12/09/2019

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Bukoba Mjini anapenda kuwajulisha kuwa, zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 litafanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 8 Octoba, 2019 hadi tarehe 14 Octoba, 2019 katika Mitaa yote ya Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba. Na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 utafanyika tarehe 24 Novemba, 2019.

Katika zoezi la Uandikishaji Wapiga Kura na Uchaguzi watatumika *Waandishi Wapiga Kura na Wasimamizi wa Vituo vya kupigia Kura*. Hivyo anakaribisha maombi kutoka kwa Watumishi wa Umma wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo;

1. Sifa za Mwombaji wa nafasi ya Mwandishi Wapiga Kura na Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura
 - Awe mkazi wa kawaida wa Kata husika anayoombea.
 - Awe ni mtumishi wa Umma isipokuwa Mtendaji wa Kata au Mtaa
 - Asiwe kiongozi au kada wa Chama cha Siasa.
 - Awe mwadilifu na mwaminifu.
2. Majukumu ya Mwandishi Wapiga Kura na Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura
 - Kuhakikisha kuwa kituo kinafunguliwa kwa wakati na kuanza uandikishaji na upigaji Kura kwa muda uliopangwa.
 - Kubandika bango la Kituo cha Kuandikisha Wapiga Kura na Upigaji Kura na mabango mengine yaliyotolewa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kituo.
 - Kuhakikisha vifaa muhimu vya kituo vinakuwepo katika Kituo.

- Kuwepo kituoni muda wote wa kazi hata kama hakuna Wapiga Kura wanaokuja kujiandikisha au Kupiga Kura.
- Kuwa makini katika Uandikishaji na Upigaji Kura ili kuepusha makosa.
- Kuhakikisha kuwa vifaa na nyaraka vinatunzwa vizuri kipindi chote na kuvikabidhi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi vikiwa katika ubora wake na,
- Majukumu mengine atakayopangiwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

- **Mambo ya kuzingatia wakati wa kutuma maombi**

- Mwombaji lazima aainishe kazi anayoomba kati *Mwandishi Wapiga Kura* na *Msimamizi wa Kituo cha kupigia Kura* au zote kwa pamoja.
- Mwombaji lazima kupitisha maombi yake kwa Msimaizi wake wa kazi ya Karibu.
- Mwombaji lazima ainishe kazi yake na Kituo cha kazi
- Mwombaji lazima abainishe namba yake ya simu
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **23/09/2019**.
- Maombi yote yatumwe kupitia anuani ifuatayo;

- **MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
JIMBO LA BUKOBA MJINI
S.L.P 284,
BUKOBA.
TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA,



Richard M. Mihayo
 MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
 JIMBO LA BUKOBA MJINI